

Jina _____, Nambari yako _____

7015/2
KISWAHILI
DISEMBA 2013
Muda: Saa 1 $\frac{1}{2}$

Sahihi ya Mtahiniwa _____

Tarehe _____



THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

CERTIFICATE IN EARLY CHILDHOOD DEVELOPMENT AND EDUCATION

KISWAHILI

Muda: Saa 1 $\frac{1}{2}$

MAAGIZO

*Karatasi hii ina sehemu tatu: Insha, Ufahamu na Lugha.
Chagua insha moja kati ya mbili ulizopewa.
Jibu maswali yote.*

Kwa matumizi ya mtahini pekee

Swali	Upeo	Alama
1	15	
2	15	
3	20	
Jumla	50	

Karatasi hii ina kurasa 7 zilizopigwa chapa.

**Watahiniwa ni lazima wahakikishe kuwa kurasa zote
zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

SEHEMU YA KWANZA: INSHA (Alama 15)

Jibu swali la 1 au la 2.

Andika insha moja isiyopungua maneno 300 kuhusu mojawapo wa mada zifuatazo;

1. Mtoto ni mtoto awe wa kike au wa kiume.
2. Anza kwa:
“Niliangalia huku na huku bila ya kusadiki niliyoyashuhudia...”

www.atikaschool.com

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.

Mwalimu wa chekechea ni muhimu sana katika elimu. Katika ulimwengu huu ambao kila mtu **anapania** kupata maarifa na tajriba kubwa iwezekanavyo, msingi bora wa masomo unafaa kutiliwa mkazo. Hivyo basi, kila mwalimu anayefunza chekechea anastahili kuwa mtu aliyehitimu vizuri katika taaluma hiyo.

Ni dhahiri shahiri kuwa majukumu ya mwalimu wa chekechea ni mengi. Mbali na kufunza mtoto stadi za kimsingi za kusikiliza na kuongea, mwalimu huyu hutarajiwa pia kuyashughulikia mahitaji mengine ya mtoto. Ikizingatiwa kuwa watoto wengine hupelekwa shule wakiwa wabichi, mwalimu hutarajiwa kuwafunza mambo ya kimsingi kama vile adabu na jinsi ya kuingiliana na wenzao. Huwafunza kuwa karimu, na kuwakubali watoto wengine bila kujali **usuli** wao kijamii na kiuchumi. Huwafunza pia kusameheana wanapokosana. Isitoshe, watoto wanapougua au kuumia wakiwa shuleni wamo mikononi mwa mwalimu. Mwalimu huyu hana budi kujiwekea kijisanduku cha huduma ya kwanza ili kuwafaa watoto inapotokea dharura.

Pamoja na majukumu haya, mwalimu wa chekechea anakabiliwa na changamoto anuwai. Baadhi yao hulipwa mishahara duni. Jambo hili humfisha sana mwalimu moyo na huweza kuathiri utendaji kazi wake. Athari hii huweza kuonekana wazi katika masomo ya watoto. Watoto huweza kukosa msingi mzuri wa masomo na kwa hivyo kufeli mitihani yao ya halafu.

Nia na azma ya Tume ya Kuajiri Walimu nchini ya kufikiria kuwaajiri walimu wa chekechea inafaa kupokelewa kwa mikono miwili na kwa moyo mkunjufu. Hili litakapotimia, kila shule ya msingi nchini itanufaika na mwalimu wa chekechea. Hadhi ya mwalimu wa chekechea pia itapanda. Mshahara wa mwalimu utaimarika. Atajiona mdau halisi katika mfumo wa elimu na kwa hivyo kutoa mchango wake kwa **udi na uvumba**. Ataionea kazi yake fahari na kujiona mtu wa maana katika jamii.

Maswali

- (a) Huku ukirejelea taarifa, eleza umuhimu wa mwalimu wa chekechea katika malezi.

(alama 6)

- (b) Andika athari **sita** zinazotokana na kutokuwepo na tume maalum ya kuwaajiri walimu wa chekechea.

(alama 6)

- (c) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika taarifa.

- (i) anapania

(alama 1)

(ii) usuli.

(alama 1)

(ii) udi na uvumba.

(alama 1)

SEHEMU YA TATU: MATUMIZI YA LUGHA (Alama 20)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

(a) Ainisha maneno katika sentensi ifuatayo;
Mwalimu mzuri amewasili mapema.

(alama 2)

(b) Tunga sentensi **tatu** kubainisha matumizi matatu tofauti ya **ji**.

(alama 3)

(c) Andika sentensi ya kauli ya kutendea inayoonyesha kuwa jambo limefanywa kwa sababu ya jingine au mtu mwingine.

(alama 2)

(d) Tunga sentensi ukitumia nomino inayotokana na kitenzi: oa.

(alama 2)

(e) Akifisha sentensi ifuatayo:

Mama mama mbwa ananibwekea aliita mtoto

(alama 3)

(f) Fafanua maana **mbili** za kauli ifuatayo:

Amekuja kutuliza.

(alama 4)

(g) Andika nahau inayoweza kumrejelea mtu ambaye anawanyima watu kitu ingawa hana haja nacho.

(alama 1)

(h) Andika methali iliyo kinyume na “mwenda pole hajikwai.”

(alama 2)

(g) Mali inayolipiwa mke huitwa _____.

(alama 1)